Sura ya 11 - Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ubatizo katika Roho Mtakatifu

Katika Luka 3:16 Yohana Mbatizaji alisema, "…mimi nawabatiza kwa maji, lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto."

Waamini wengi hawatambui baadhi ya mambo muhimu ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika Yohana sura ya 14, 15 na 16. Alifahamu kwamba atauawa na kwamba atafufuka. Alijua pia kwamba atarudi tena kwa Baba lakini atamtuma Roho Mtakatifu kuchukua nafasi yake.

Aliyasema haya yafuatayo akijua jinsi watakavyojisikia hawana baba wasipouona uwepo wake. "Sitawaacha ninyi yatima [bila baba]; naja kwenu" (Yohana 14:18).

Aliwaambia kabla hajapaa mbinguni kwamba watajazwa Roho Mtakatifu. "Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache (Matendo ya Mitume 1:5). "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo ya Mitume 1:8).

Aliwaambia wasiogope yeye atakapoondoka. Aliwaeleza kwamba Roho Mtakatifu atachukua nafasi yake na kumfanya yeye (Yesu, Mungu) adhihirike katikati yao. Soma maneno ambayo Yesu aliwaambia katika Yohana 14:16-26).

Yesu aliwaambia kwamba Roho Mtakatifu atamdhihirisha Yesu katikati yao.

Naamini hili ndilo lengo kuu la Ubatizo katika Roho Mtakatifu

"Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia" (Yohana 15:26).

"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu" (Yohana 16:7).

Yesu aliwaambia watu wake kwamba atakuja upesi. Na kweli alikuja! Alikuja kwa njia ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu na Yesu siyo watu tofauti, ni wamoja ila tu katika sura tofauti. Roho Mtakatifu huweza

kuishi ndani ya wanadamu, wakati ambapo Yesu alikuwa katika mwili mmoja tu.

Wanafunzi wa Yesu walipata uzoefu wa mambo mawili kuhusu Roho Mtakatifu. Wanafunzi wale wa kwanza walimpokea Roho Mtakatifu wa Yesu aliyefufuka katika Yohana 20:22. Hata hivyo wanafunzi hao hao hawakuweza kuona badiliko lolote la tabia hadi walipompokea Roho Mtakatifu wa Kristo aliyepaa mbinguni, siku ya Pentekoste katika Matendo ya Mitume sura ya 2.

A. Jumapili ya Ufufuo, Yohana 20:22.
Kristo aliyefufuka.
Katika Roho ya uvuvio.
Matokeo yalikuwa uzima.

B. Jumapili ya Pentekoste, Matendo ya Mitume 2:4.
Kristo aliyepaa mbinguni na kutukuzwa.
Roho aliyemiminwa.
Matokeo yalikuwa nguvu.

Lile kundi la watu 120 katika Matendo ya Mitume sura ya 2 lilijiachia na kuzama katika uwepo wa Mungu. Walitumia muda na kuongea maneno ya urafiki wa karibu. Walipokea nguvu iliyobadilisha maisha yao, nguvu ya kushuhudia, nguvu ya kupokea mahitaji yao yote, nguvu ya kueneza ufalme wa Mungu katika maeneo mengine na nguvu ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu na ushirika na Kristo aliyetukuzwa, kila siku.

Yesu sio tena mtu anayetembea juu ya Bahari ya Galilaya, wala sio mtu anayeteseka msalabani, na wala sio mtu aliyefufuka tu. Sasa yuko tofauti! **Hakuna mwanadamu aliyemuona Yesu katika hali hii**, isipokuwa Yohana katika kisiwa cha Patmo kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana. Soma Ufunuo wa Yohana sura ya 1.

Wanafunzi wa Yesu walipata uzoefu wa kitu fulani siku ile ya Pentekoste, kitu ambacho sisi sote tunahitaji kukipata. Yesu aliporudi mbinguni katika Matendo ya Mitume sura ya 1, alichukua nafasi mpya kuwa Kristo aliyepaa, na sio tu Kristo aliyefufuka. Yesu aliondoka duniani katika umbo la aliyefufuka, lakini alirudi tena katika Roho Mtakatifu akiwa mwenye nguvu zaidi, aliyepaa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu na aliyetukuzwa.

Angalia, wanafunzi wake hawakuhuzunika katika Matendo ya Mitume sura ya 1-3 kama walivyofanya katika kitabu cha Yohana aliposulibiwa. Wakati huu, alipoondoka, waliliamini neno alilowaahidi kwamba atarudi upesi katika nafsi nyingine. Na hazikupita siku nyingi baada ya yeye kuondoka, alirudi tena kama Roho Mtakatifu, na walijazwa. Kisha waliendelea kuishi maisha yao wakiwa na ushirika na Yesu kana kwamba alikuwapo pamoja nao (Alikuwa pamoja nao).

Kubatizwa maana yake kuzamishwa. Kwanza tulibatizwa kwa maji na sasa kwa moto. Moto ni uwepo wake. Tunapobatizwa katika maji tunakuwa

tumekufa, tumeaibishwa, lakini maji hayaingii ndani yetu na kutuua kabisa. Ni kwa nje tu. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni moto wa Mungu unaoingia ndani yetu. Ni chaguo letu. Tunaweza kuchagua kiburi chetu kitawale badala ya kuwa na uwepo wake au badala ya yeye kututawala. Lakini yeye anataka kuteketeza utu wetu wa kale kwa moto. Mungu alimuahidi Nuhu kwamba maji hayatakuwapo tena, bali moto tu. Pepo huharibiwa na moto siyo maji.

Je, tunahitaji kujazwa zaidi ya mara moja? Baadhi ya madhehebu wanapinga jambo hili na kukosa ukweli. Sisi sio kama bilauri inayojazwa maji kwa kutumia gudulia au jagi. Kama hii ingekuwa kweli labda tungehitaji kujazwa tena na tena kwa sababu kuna uwezekano wa kuvuja.

Neno la Mungu katika Yohana 15 linasema kwamba tumeungana na Yesu kama tawi la mzabibu. Suala muhimu siyo kujazwa mara kwa mara, bali ni kukaa ndani yake wakati wote. Utomvu ndani ya mzabibu unawakilisha Roho Mtakatifu. Yesu ni mzabibu na sisi ni matawi. Tunahitaji kukaa ndani ya mzabibu. Yesu anasema kwamba kutii Neno lake ndilo jambo linalotuwezesha kukaa ndani yake wakati wote. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni kufurikwa na uwepo wa Mungu tunapokuwa tumeunganishwa na Yeye kama mzabibu na tawi. Utomvu wake hutiririka ndani yetu, na hivyo tunaendelea kuungana na Yeye tukikaa ndani yake.



Kiasi gani cha ujazo kinatosha? Neno la Mungu katika Luka 6:45b linasema hivi: “Kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake.” Mimi binafsi napenda wazo hili kwamba Roho Mtakatifu anatiririka kutoka katika kinywa changu akiniambia kwamba nimejazwa!

Kumekuwa na utatanishi na mabishano mengi kuhusu Ubatizo katika Roho Mtakatifu. Baadhi ya watu husema kuwa karama za Roho ndilo

jambo muhimu na wengine husema kwamba jambo muhimu ni kunena kwa lugha. Na wengine nao wanasema kwamba ubatizo ni kwa ajili ya huduma, na kwamba kama kweli tunahitaji kumtumikia Yesu na kushuhudia kwa nguvu za Mungu, tunahitaji kujazwa Roho Mtakatifu. Hawajakosea, wote wana sababu nzuri, lakini siamini kwamba wamegusa kusudi la msingi la ujazo wa Roho Mtakatifu.

Vipi kuhusu karama za Roho?

Ninaona kwamba ni vizuri tuliache suala la utoaji wa karama kwa mtoaji mwenyewe. Mimi binafsi nimekuwa na karama nyingi zikitenda kazi katika maisha yangu mara kwa mara, lakini siyo zote.

Ninaamini kunena kwa lugha kwamba ni karama muhimu na ya thamani. Mungu huitumia sio tu katika huduma inayofanyika katika kundi la watu, bali pia hutawala mioyo yetu kwa faida yake. Yakobo alisema kwamba ulimi ni kama usukani mdogo sana unaoongoza merikebu yote. Kama unataka kumpa Yesu usukani wa maisha yako, mpe ulimi wako. Kuna mafundisho kamili juu ya jambo hili katika mtaala wa ISOB unaoitwa "Roho Mtakatifu na ulimi."

Sio vizuri watu waliopokea karama kuwafanya wale ambao hawajapokea wajisikie kana kwamba wamefanya kosa fulani. Na pia sio vizuri kwa watu ambao hawajapokea karama kuwahukumu walio nazo. Yesu, katika Mathayo 12:31, anaonyesha wazi kwamba kukufuru kazi anazozifanya Roho Mtakatifu ni njia ya uhakika ya kukosa kupokea baraka hizo katika maisha yako mwenyewe. Kumkufuru Roho Mtakatifu ni kusema kwamba jambo fulani halitokani au halijafanywa na Roho Mtakatifu wakati ni kweli jambo hilo limefanywa na Roho Mtakatifu. Kama huna uhakika, sawa, lakini uwe mwangalifu usiseme kinyume na jambo hilo isipokuwa tu kama una uhakika kabisa na unao uthibitisho kwamba jambo fulani ni la kishetani. Ni vizuri ujihadhari vinginevyo utakuja kujilaumu!

Yesu anawezaje kutimiza yote aliyotuahidi asipodhihirika kwetu? Roho Mtakatifu humdhihirisha Yesu kwetu ili aweze kufanya yale yaliyoahidiwa katika Isaya 61.

Mungu anataka kutuweka huru mbali na utumwa wa aina mbalimbali. Hata hivyo, uhuru sio lengo kuu. Lengo kuu ni kutupatia uhuru ili tuweze kuingia katika uwepo wake na kuwa na ushirika naye, jambo ambalo litatufanya tuzae matunda kwa ajili ya maisha yetu na kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

1. Uhuru kutoka katika utumwa → 2. Kufurahia Uwepo wake na kuzaa matunda

Katika kitabu cha Kutoka, Mungu alimtumia Musa kuwatoa watu wake Israeli katika utumwa wa Misri na Farao. "Wape watu wangu ruhusa waende, ili kunifanyia sikukuu jangwani" (Kutoka 5:1b). Uhuru kutoka Misri halikuwa suala kubwa, kitu muhimu kwa Mungu ni "sikukuu jangwani." Au kwa maneno mengine, ushirika pamoja naye katika uwepo wake.

1. Uhuru kutoka katika utumwa

Yesu alidondoa Isaya 61 katika Luka 4:18 wakati alipotangaza kusudi la huduma yake. Isaya 61 inaanza na maneno anayosema Yesu kwamba Roho ya Bwana MUNGU amemtia mafuta awahubiri wanyenyekevu habari njema; amemtuma awagange waliovunjika moyo. Yesu anatangaza uhuru kwa mateka, anafungua magereza kwa wale waliofungwa, na kutangaza "Mwaka wa Bwana uliokubaliwa" au "Mwaka wa jubilii" (wakati ambapo watumwa huwekwa huru). Anaendelea kuorodhesha mambo mengine mengi yatakayofanywa na huduma yake.

Anasema kwamba wafungwa hawa na wanyenyekevu watabadilishwa na kuwa miti ya haki, watakuwa na nguvu na pia watampendeza Mungu. Anasema kwamba hawatakuwa tena na roho nzito kwa sababu ya maombolezo bali watajazwa furaha.

Kisha anasema kwamba watajenga upya mahali palipoharibiwa. Kwa maneno mengine maisha yao yaliyoharibiwa yatajengwa upya, kama Nehemia (ambaye jina lake linamaanisha mfariji au Roho Mtkatifu) aliyejenga upya kuta za Yerusalemu zilizokuwa zimebomoka. Vile vile, alisema kwamba mahitaji yao yote yatashughulikiwa na kwamba watakuwa makuhani wa Mungu, au wawakilishi wake binafsi. Kisha na wao watawakomboa wengine na kuwaweka huru.

Kwa muhtasari Isaya 61 inaeleza kwamba Yesu atawabadilisha watu kutoka katika hali ya kuwa wafungwa hadi kuwa makuhani kwa njia ya Roho Mtakatifu. Hivi ndivyo tulivyosema katika Sura ya 1 ya kitabu hiki, kwamba tutazaa matunda katika maeneo yote matatu ya maisha yetu; tabia zetu, mahitaji yetu na huduma zetu kwa wengine. Kutoka hali ya kuwa wafungwa hadi kuwa makuhani.

"Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta:

1. niwahubiri wanyenyekevu habari njema,
2. amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo,
3. kuwatangazia mateka uhuru wao,
4. na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao" (Isaya 61:1).
5. "kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa na
6. siku ya kisasi cha Mungu wetu;
7. kuwafariji wote waliao;" (Isaya 61:2).
8. "kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu,
9. mafuta ya furaha badala ya maombolezo,
10. vazi la sifa badala ya roho nzito;
11. wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA , ili atukuzwe"(Isaya 61:3).
12. "Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani, watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi" (Isaya 61:4).
13. "Na wageni watasimama na kulisha makundi yenu, na watu wa kabila nyingine watakuwa wakulima wenu, na watunzaji wa mizabibu yenu" (Isaya 61:5).
14. "Bali ninyi mtaitwa makuhani wa BWANA; watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wetu; mtakula utajiri wa mataifa, na kujisifia utukufu wao" (Isaya 61:6).
15. "Badala ya aibu yenu mtapata maradufu, na badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao; basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele" (Isaya 61:7).

Yesu aliahidi kufanya yote hayo kwa ajili yetu sote, lakini hayupo tena hapa duniani. Alimtuma mfariji mwingine, Roho Mtakatifu, achukue nafasi yake. Roho Mtakatifu ndiye sasa anayesimamia na kutoa ahadi hizi kwetu. Hatuwezi kupata baraka zote hizo tusipokuwa na ushirika na Yesu kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Tunahitaji Yesu adhihirike kwetu. Tunahitaji kuungana naye ili tupate yote aliyoyaahidi katika Isaya 61. Mambo yanapokwenda kombo katika maisha yetu, tukimsikia Yesu anasema nasi, kila kitu kitakuwa sawasawa!

Kama tu wafungwa, na kama tu wanyenyekevu, waliovunjika moyo na kupigwa, hatuhitaji kungojea twende mbinguni ili tupate msaada; tunahitaji msaada huo SASA! Tunaweza kuupata sasa katika maisha haya, lakini lazima tuwe na ushirika na Mungu. Anahitaji kujidhihirisha kwetu. Anahitaji kuwa zaidi ya dini, zaidi ya mafundisho ya dhehebu letu, zaidi ya maneno ya Maandiko Matakatifu (kama jinsi yalivyo muhimu). Tunahitaji kuwa na ushirika na Yesu aliye hai kama jinsi wanafunzi wake walivyokuwa wakati Yesu alipokuwa duniani, na kama jinsi walivyoendelea kuwa na ushirika naye hata baada ya yeye kupaa mbinguni, kama tunavyoona katika Matendo ya Mitume.

Neno la Mungu katika Waefeso 3:18-19 linasema, "ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu."

Mungu alidhihirika kwa Yakobo katika Mwanzo sura ya 28. Yakobo alionja uwepo wa Mungu na hakupenda kuuachia! Maneno ya Mungu katika Mwanzo sura ya 28 mstari wa 10-17 yanaelezea jinsi Yakobo alivyosikia uwepo wa Mungu wakati alipoota ndoto kuhusu ngazi inayounganisha mbingu na nchi. Asubuhi iliyofuata, Yakobo aliamka na kujenga madhabahu pale na kuiita Betheli, yaani nyumba ya Mungu. Alikuwa amekamatwa kikamilifu na hali nzuri ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu. Mungu alidhihirika kwake. Yakobo alikuwa kama wewe na mimi. Alihitaji mabadiliko makubwa. Utu wake wa asili ulikuwa umeharibika. Ili kumbadilisha Yakobo, Mungu alimvuta awe na urafiki wa karibu pamoja naye. Mungu akajidhihirisha kwa Yakobo. Yakobo akampenda sana Mungu, na kumfuata maisha yake yote. Baadaye, walipokuwa wakitembea pamoja, Yakobo alibadilishwa kutoka Yakobo na kuwa Israeli.

Kabla Yesu hajaingia katika maisha yangu, nilikuwa kweli mfungwa wa kiroho. Kulikuwa na pepo waliokuwa wakitawala maisha yangu. Nilipomuona Yesu katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana kama Kristo aliyepaa mbinguni, mshindi na mkombozi, nikapata kuwa mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Hiii ilitokea tarehe 26 mwezi Agosti, mwaka 1979. Yesu alidhihirika wazi kwangu kama ninavyomuona jirani yangu. Alisema na mimi na kunisikiliza. Alikuwa pamoja nami katika maumivu na shida zangu. Watu waliponidhihaki, alinifariji. Watu walipojaribu kunifanya mateka, alinifundisha kweli iliyoniweka huru. Baada ya muda mfupi, kama Isaya anavyosema katika sura 10:27, nira yangu (ya kukandamizwa na kuteseka) shingoni mwangu iliharibiwa, kwa sababu ya kutiwa mafuta.

Kidogo kidogo, Yesu aliniweka huru mbali na pepo waliokuwa wakiniathiri na kunishika na pia wale waliokuwa wamefanya mwili wangu kuwa "nyumba" yao. Nilipofanya ushirika na Yesu katika Neno na kwa njia ya maombi, niliweza kulia bila kujizuia, machozi na makamasi yalinitoka sana. Tunasoma katika Luka 11:24 kwamba pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji (mahali pakavu) akitafuta mahali pa kupumzika; asipoona hutafuta kurudi tena mahali palipo na "maji." Mahali palipo na maji, nyumba yao ya kwanza, ni mtu. Na sehemu kubwa ya mwili wa mtu ni maji. Ukombozi huu uliendelea kila wiki kwa kipindi cha miezi kadhaa, au hata miaka - siwezi kukumbuka.

Siku zilivyoendelea, niliwekwa huru mbali na pepo walionifanya mateka. Tabia yangu ikaanza kufanana na tabia ya Yesu. Nikaanza kupata mahitaji yangu. Mungu akanipa chaguo lake la mke na familia.

Baada ya miaka mingi ya nidhamu, amenifanya kuwa mhudumu wa Mungu, kama alivyoahidi katika Isaya 61. Mungu alimtumia Roho Mtakatifu kuleta mabadiliko haya katika maisha yangu. Naye Roho Mtakatifu akamdhihirisha Yesu kwangu. Yesu hakufanya hivyo, bali Roho Mtakatifu ndani yangu aliyeondoa kila kitu kisicho cha Mungu.

2. Kufurahia uwepo wake na kuzaa matunda.

Baada ya uhuru kutoka katika utumwa, Mungu anataka tupate uzoefu wa uwepo wake na Ufalme wake

Roho Mtakatifu hufanya Ufalme wa Mungu udhihirike kwetu katika maisha haya. Waebrania 12.

Maandiko ya wazo kuu au dhamira ya Sehemu hii ya Pili yanatoka katika Waebrania 12. Sura hii inazungumzia kupiga mbio, lakini pia inazungumzia kuweka kando kila mzigo na dhambi. “Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu” (Waebrania 12:1).

Sura hii inaendelea kuzungumzia juu ya ukweli wa mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, uitwao pia mlima Sayuni. Inavyoonekana, kuweka kando dhambi na kila mzigo, na kufuata mengine yote yaliyoelezwa katika waebrania 12 ni kuufanya ufalme wa Mungu udhihirike katika maisha yetu.

Hebu tuchunguze yale aliyoyasema mwandishi wa kitabu hicho cha Waebrania kwa watu wale kuhusu kupiga mbio, kuweka kando kila mzigo mzito na dhambi na ufalme wa Mungu kudhihirika kwetu.

1. Katika Waebrania 12:2-4 tunaambiwa kwamba tunapaswa **kusimama kwa uvumilivu**, bila kuchoka. Tunapaswa kuvumilia mapingamizi, kutokueleweka na mateso. Kusimama kwa uvumilivu pamoja na Yesu ni kuotesha mbegu mioyoni mwetu kwa ajili ya kuzaa matunda.

2. Katika Waebrania 12:5-11 tunaambiwa kwamba Mungu **ataturudi**, sio kutupiga, bali kutusahihisha kama wana kwa upendo na kwa faida yetu wenyewe. Ni kweli tunahitaji kurudiwa na Mungu. Kuna mambo mengine tusiyoyaona.

Yakobo alikuwa na ubinafsi tena mkaidi. Mungu alimrudi kwa njia ya mazingira hadi jina lake lilipobadilishwa kutoka Yakobo na kuwa Israeli, na kutoka mlaghai kuwa mtu anayeshindana na Mungu.

Tunahitaji kuyaona mazingira yetu kuwa yamepangwa na Mungu ili kwamba tunapopita katika mazingira hayo, mwenendo wetu ubadilishwe ufanane na wake. Hii haina maana kwamba Mungu huleta mazingira au mambo mabaya katika maisha yetu. La hasha; Shetani ndiye

anayefanya hivyo. Lakini, unaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu anayatumia mazingira hayo kutufanya tufanane naye. Mungu hutumia Neno lake kuturudi, lakini kuna maeneo ya utu wetu wa kale yanayohitaji kwanza kupitia katika majaribu ili yasafishwe.

3. Katika Waebrania 12:12 na 13 tunatiwa moyo tusonge mbele wakati hali sio nzuri.

4. Katika Waebrania 12:14 tunaambiwa tutafute kwa bidii amani na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.

5.Tunaambiwa katika Waebrania 12:15-16 tusiipungukie neema ya Mungu na pia tujiepushe na uchungu. Tunaambiwa pia tusiwe kama Esau aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza na hakuweza tena kutubu.

6. **Sasa, hii hapa ni thawabu**. Soma Waebrania 12:18-29. Mmeufikilia mlima Sayuni, ufalme wa kiroho, Ufalme wa Mungu. Ni sasa, sio tu wakati ujao. Mungu anataka tuishi katika ufalme wa mbinguni, sasa hivi wakati bado tupo duniani. Tunaweza kuishi katika "zamani zijazo," (Waebrania 6:5), lakini tunahitaji kwanza kujazwa Roho Mtakatifu. Anataja kwamba mlima Sayuni, au ufalme wa Mungu, una sifa kadhaa.

a. **Kwanza, ni Mungu aliye hai.** Roho Mtakatifu anatuwezesha kuwa na ushirika na Mungu aliye hai sasa kwa sababu yupo hapa pamoja nasi.

b. **Pili, ni Yerusalemu wa mbinguni.** Roho Mtakatifu anatuwezesha kuishi katika ufalme wa Mungu, sasa.

c. **Kisha, malaika wanatajwa**. Hatuhitaji sana kulenga macho yetu kwa malaika, lakini tunahitaji kujua kwamba wapo hapa ili kupigana vita kwa ajili yetu na wanafanya hivyo kwa Neno la Mungu.

d. **Tumelifikia kanisa** la Mzaliwa wa kwanza, Yesu, wale walio raia wa mbinguni. Hii inatuonyesha kwamba tunapaswa kukaa katika kanisa zuri linaloamini Biblia na ambalo limejazwa Roho.

e. **Mungu, Mwamuzi** anatajwa katika mstari wa 23. Ninafurahi kwamba Mungu ni mwamuzi wangu; hiyo inamfanya Mwokozi wangu awe pia mwamuzi wangu. Yeye anatufanya tuone makosa yetu ili tutubu na kushinda. Vile vile, Mungu ni hakimu wa adui yetu, Shetani. Amekwisha mhukumu Shetani. Mungu atakuhukumu wewe mwenye haki na kumhukumu pia Shetani katika kila eneo la maisha.

f. Waebrania 12:23 inataja roho za watu wenye haki waliokwenda mbinguni. Siamini kwamba ninaweza kuwasiliana na roho za watakatifu waliotutangulia, lakini ninaamini kwamba wanatuona. Tunaonwa na kushangiliwa na wingu kubwa la mashahidi. Ushuhuda wa imani yao ndio tunaouona.

g. Katika Waebrania 12:24 tunaambiwa kwamba tunaye **Yesu mjumbe** wa Agano la damu. Tunamshukuru Mungu kwa hili. Yesu sio tu kwamba anafanya agano la damu pamoja nasi, lakini pia alifufuliwa kutoka katika wafu ili awe mpatanishi na mdhamini wa agano. Tunapofanya makosa, Yesu hutuwezesha kuungama na kutubu dhambi zetu na kisha hutupatanisha na Mungu. Ni mpatanishi na wakili wetu. Anahakikisha kwamba tunashinda.

h. Katika Waebrania 12:25 tunaonywa tusimkatae yeye anenaye, vinginevyo hatutaokoka tukijiepusha na yeye atuonyaye.

i. Katika Waebrania 12:26-28 tunaambiwa kwamba **Mungu atatetemesha** kila kitu mbinguni na duniani, ili kwamba vile vitu vinavyotakiwa kuondolewa, viondolewe na vile ambavyo vimesimama imara, katika ufalme wa Mungu, vitashinda jaribu hilo na kuendelea kusimama imara.

j. Mwisho, katika Waebrania 12:29 tunaambiwa kwamba **Mungu ni moto ulao.** Moto ulao ni Roho Mtakatifu. Amekuja kutukomboa kutoka katika yale yote yanayoweza kutetemeshwa, na pia kutoka katika masazo ya utu wa kale, mwili na hali ya dhambi.

Tufanyeje ili tushirikiane na Mungu?

1. Tunahitaji kuwa na njaa ya kuona Mungu akijidhihirisha kwetu. Wale watu 120 orofani walikuwa baadhi tu ya watu ambao Yesu alikuwa amejidhihirisha kwao baada ya kufufuka. Kulikuwa na watu wapatao 500. Kitu gani kilitokea kwa hao wengine? Labda hawakuwa na njaa ya kutosha. Au labda walijivuna sana au huenda walikuwa wamefungwa na shughuli zao au na familia zao. Inawezekana pia walikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi watu wengine watakavyowafikiria. Kumbuka wale 120 walishutumiwa na kuchekwa.

2. Tunahitaji kuwa na mizizi katika Neno ili tuwe washindi. Agano la damu huondolewa kwa maneno na siyo damu. Neno likijaa kwa wingi ndani yako, utakuwa na damu nyingi pia, na pia maisha yako yatajaa tabia ya Kristo. Kwa jinsi hiyo dhambi zako zitaondolewa kwa wingi. Pepo hawatakuwa na athari kwako. Utajazwa Roho Mtakatifu. "Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo" (Yohana 3:34).

3. Tunahitaji kujiandaa kukataliwa na ukoo wetu au dhehebu letu. Katika Luka 12:49-52 imeandikwa hivi: "Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi? Lakini nina ubatizo unipasao kubatizwa, nami nina dhiki kama nini hata utimizwe! Je! Mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, La, sivyo, bali mafarakano. Kwa kuwa tokea sasa katika nyumba watakuwamo watu watano wamefarakana, watatu kwa wawili, wawili kwa watatu."

4. Tunahitaji kuwa wazi kwa Yesu na kumwamini. Katika Luka 11:11-13 tunaambiwa hivi: "Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"

5. Roho Mtakatifu kila wakati anaheshimu toba. Huonekana tunapotubu dhambi na kuyaacha mambo ya ulimwengu, kiburi na uvivu wetu. Katika Matendo ya Mitume 26:18 imeandikwa hivi, "uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi."

6. Tunampokea Roho Mtakatifu kwa imani. Imani katika nini? Yesu alizungumzia ujazo wa Roho Mtakatifu katika Yohana 7:38-39, "Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa **hajatukuzwa.**"

Kwa hiyo Yesu alihitaji **kutukuzwa** kwanza kabla hatujawa na imani ya kumpokea Roho Mtakatifu kama mafuriko ya mto ulio hai. Kutukuzwa maana yake nini? Kutukuza ni neno linalomaanisha kufunua au kuweka wazi kitu cha kweli. Ni kama mtu anayeondoa kitambaa kilichofunika sura ya kitu fulani na kuionyesha wazi sura hiyo kwa mara ya kwanza.

Katika Yohana 17:4-5 Yesu alimwomba Baba, akisema, "Mimi **nimekutukuza** duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. Na sasa, Baba, **unitukuze** mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako." Yesu alimfunua Baba kwa watu aliokutana nao. Sasa ilikuwa zamu ya Baba kuonyesha Yesu alikuwa nani hasa.

Yesu alitukuzwaje? Kumbuka, kutukuza maana yake ni kuonyesha sura ya kweli au sura halisi ya mtu au kitu. Katika Luka 24:13-27 alikuwa akizungumza na watu wawili katika njia ya kwenda Emau. Akasema, "Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika **utukufu** wake? Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo

yaliyomhusu yeye mwenyewe" (Luka 24:26,27). Kisha wale watu wawili walisisimka sana na walipowaona mitume 11 walianza kuwaambia yale ambayo Yesu ameyafunua. Ghafla Yesu aliyefufuka alitokeza katika mkutano huo akaanza kunena nao. "Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia , Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu" (Luka 24:44-46).

Aliwapa ufunuo au alijitukuza mwenyewe katika vitabu vya Musa, Zaburi na Manabii. Alikuwa akizungumzia vitabu vitano vya Musa, vitabu vya Manabii na Zaburi.

Hatimaye baada ya hayo, siku ya Pentekoste iliwadia wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu na moto!

Alijitukuza mwenyewe katika vitabu vya Musa:

Katika Mwanzo alijitukuza kama muumbaji. Alijionyesha mwenyewe kuwa muenezaji wa jamii mpya kwa njia ya agano la damu ili kuchukua nafasi ya jamii ya Adamu iliyoanguka dhambini.

Katika Kutoka, alijionyesha kama mtoa sheria na kama Kondoo wa Pasaka kwa ajili ya sheria zilizovunjwa. Yeye ndiye aigawanyaye bahari ya shamu ya maisha yetu na kututoa katika vifungo vya ulimwengu.

Katika Mambo ya Walawi, yeye ndiye aliyefanya agano la damu, na ndiye anayetuomba kwamba tuchukue msalaba wetu na kuishi katika utakatifu.

Katika Hesabu, yeye ndiye atupaye mahitaji yetu katika jangwa la maisha yetu; yeye ndiye mana yetu kutoka mbinguni na maji kutoka mwambani.

Katika Kumbukumbu la Torati, ni yeye anayetukomboa kutoka katika laana ya sheria.

Alijitukuza mwenyewe katika Zaburi:

Katika Zaburi, ni mchungaji wetu tunayeweza kumtwika masumbufu yote ya mioyo yetu kwa unyofu bila kukemewa, kama Daudi alivyofanya.

Alijitukuza mwenyewe katika Manabii:

Katika Isaya ni Mwokozi anayeteseka anayechukua dhambi na magonjwa yetu.

Katika Yoeli, anaonyesha ahadi ya ubatizo katika Roho Mtakatifu. Hata hivyo kabla ya ahadi katika Yoeli sura ya 2, alionyesha hali inayotakiwa ya kujiweka wakfu kabla ya kupokea ahadi hiyo.

Aliwaonyesha pia yale niliyoyaona nilipookoka na kujazwa Roho Mtakatifu wakati huo huo, katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana kama kilivyoelezewa kabla katika kitabu cha Ezekieli na Danieli.

Katika Ezekieli 37, ni yeye anayeipa uhai mifupa yetu mikavu, kwa Roho Mtakatifu. Katika sura ya 38-39, anawashinda adui zetu. Katika sura ya 40-42 anatuonyesha hekalu la Mungu ili tujue kwamba tumekaribishwa kuwa na uhusiano wa karibu pamoja naye.

Katika Ezekieli 43, aliwaonyesha utukufu wa kiti chake cha enzi na maskani ambapo Mungu anakutana na mwanadamu kama katika Ufunuo wa Yohana 21. Katika sura ya 44-46 anatuomba tujiweke wakfu ili tuweze kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

Katika Ezekieli 47, kama katika Ufunuo wa Yohana 22, yeye ndiye anayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kusababisha mto utiririke kutoka ndani yetu hadi katika bahari ya chumvi ya wanadamu ili watu waweze kufanywa hai na Mungu.

Katika Ezekieli 48:35 jina lake ni "BWANA yupo hapa," katika Yerusalemu wa mbinguni akiishi na watu wake.

Katika Danieli sura ya 1-6 anajifunua mwenyewe kama anayetuomba tuwe ulimwenguni lakini tusiwe wa ulimwengu. Yupo pamoja nasi katika tanuru la moto na katika matundu ya simba ya maisha yetu.

Katika Danieli sura ya 7, anajionyesha mwenyewe kama mzee wa siku aliyewapa watakatifu ushindi. Katika sura ya 8-9 vita vinafananishwa na vita katika Ufunuo wa Yohana.

Katika Danieli 10:5, Anaonyesha Kristo mshindi aliyepaa mbinguni kama katika Ufunuo wa Yohana sura 10 na 11 zinavyoonyesha vita zaidi.

Danieli 12 inaelezea umuhimu wa kusimama, maana baadhi watachakazwa na adui. Sasa angalia Danieli 12:12. Watakaosimama imara hadi mwisho, watapata ushindi. Hivi ndivyo nilivyoona nilipookoka na kujazwa Roho Mtakatifu wakati huo huo mwaka 1979!

Katika Agano Jipya, Yesu alijifunua kama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Anaelezea ule utata katika Agano la Kale usemao kwamba Mungu ni mwenye rehema, husamehe dhambi lakini mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao na wana wa wana wao pia hata kizazi cha tatu na cha nne (Kutoka 34:6-7).

Alijidhihirisha mwenyewe kama Mwana wa Mungu, kama Neno la Mungu, kama Njia, Kweli na Uzima!

Alijidhihirisha mwenyewe kama Masihi atakayekuja mara ya pili kama **Mfalme mkuu katika kiti cha enzi.**

Katika Yohana 14-16, alijidhihirisha kama Roho Mtakatifu atakayekaa ndani ya wanafunzi wake.

Katika Luka 24 na Matendo ya Mitume 1 Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuyaweka wakfu maisha yao na kungojea ahadi itimie. Hii ndiyo sehemu yetu: utii, kujiweka wakfu na kujiachia.

Maombi. Bwana Yesu, Neno la Mungu linasema kwamba unahitaji kunijaza kwa Roho wako ili kwamba wewe na mimi tuzidi kuwa marafiki. Nina njaa ya kuwa na wewe na kuwa katika uwepo wako katika maisha yangu. Yesu, ninaliamini Neno lako. Ninakiri mbele zako kwamba ninahitaji kila ulicho nacho kwa ajili yangu. Njoo, Yesu, unibatize katika Roho Mtakatifu na moto. Niko wazi na niko tayari kupata moto katika maisha yangu. Nakataa na kutubu dhambi zote katika maisha yangu. Namsamehe kila mtu aliyenikosea. Najitoa kwako kuwa dhabihu iliyo hai. Wewe ni mtawala wa maisha yangu. Navitoa kwako viungo vyangu vyote, kinywa changu, ulimi wangu, mikono yangu, miguu, masikio na macho.

Vichukue vyote!

Kiambatisho A – Orodha ya Masomo ya ISOB

Orodha ya masomo ya ISOB yanayopatikana kwenye "CD ROM" kwa ajili ya Kompyuta za "Windows" au "Macintosh"

Masomo 7 ya kwanza yameambatana na sauti.

- **Kitabu cha Kukua au Kufa Sehemu ya 1**

01. Kukua au Kufa Kuzaa Matunda
02. Wafungwa katika Nchi ya Ahadi
03. Mto Utiririkao – (liendelezwe kila siku)
04. Mungu ni Nani
05. Kuketi
06. Kuenenda
07. Kupinga

- **Kitabu cha Kukua au Kufa Sehemu ya 2 (Damu na Moto)**

08. Nguvu ya Kupiga Mbio
09. Msalaba
10. Ukombozi – Pepo
11. Ubatizo katika Roho Mtakatifu

……..

4 Mungu Ni Nani
(somo moja moja)

01. Kumjua Mungu wetu wa ajabu
02. Utatu
03. Mungu Baba
04. Mungu Baba – 2
05. Mungu ni wa agano
06. Uzao Mtakatifu
07. Uzao Mtakatifu – 2
08. Yesu ni nani Sasa?
09. Sura ya Mungu
10. Mungu Neno
11. Mamlaka ya Neno la Mungu
12. Ukamilifu wa Neno
13. Utakaso Unaofanywa na Neno
14. Kristo Mwamba

15. Unabii wa Biblia –
Jina la Yesu katika Agano la Kale
16. Mungu Roho Mtakatifu
17. Roho Mtakatifu na Lugha
18. Ubatizo katika Roho Mtakatifu
----

5 Kuketi
Somo moja moja:

01. Muhtasari wa Kuketi – Kuketi na Kristo
02. Neema
03. Utambulisho
04. Upendo Mkuu
05. Nilinunuliwa toka utumwani
06. Ukombozi
07. Nani alikuambia
08. Uponyaji wa Miili yetu
09. Mizizi
10. Ushindi juu ya Dhambi
11. Hofu
12. Hatia
13. Nguvu ya kumaliza mshindano – Msalaba
…….

6 Kuenenda

01. Muhtasari wa kuenenda
02. Kurudi nyuma
03. Kijana Tajiri – Kuweka wakfu
04. Kuwa na shughuli nyingi kwa ajili ya Mungu
05. Imani
06. Samehe
07. Ulimwengu
08. Ukweli/Zaka
09. Ukweli wa Adhabu ya Kifo
10. Ukweli
11. Mamlaka
12. Tubu
13. Usomaji wa Biblia
14. Mwenendo kwa Mtu aendaye Mbinguni
15. Angalia Yasiyoonekana
16. Utumishi
17. Kuwatanguliza wengine
18. Mheshimu kwa mwili wako
19. Mwitikie Mungu
20. Linda moyo wako
21. Zaka – Uchumi
22. Maombi

23. Utumie Urithi wako
24. Enenda kwa Roho
25. Kukubaliana
26. Maneno Yako
27. Omba - Imani
28. Kurudi Nyuma
29. Rehema
30. Uwe Mkweli
31. Lawama
32. Upendo
33. bada
34. Urafiki
35. Sifa – Wimbo mpya
36. Marafiki zako
37. Ushirika na waaminio
38. Ubatizo
39. Hukumu
40. Kuchezea Neema
41. Kufunga
……..

7 Kupinga

01. Muhtasari wa Kupinga – Kuzipinga hila za Shetani
02. Damu ya Vita
03. Chumba cha Mahakama
04. Amani Iwepo
05. Ufunuo
06. Gombo
07. Matatizo
08. Imetiwa Mhuri
09. Aketipo Shetani
10. Siyo mapenzi yangu
11. Shetani, pepo, mashetani, ukombozi

Mtaala wa ISOB na kazi za darasani
Uanafunzi wa Yesu/Uongozi III

Kuwa Huru

01 Kuwa Huru
02 Majitu Yanaizunguka Ahadi yako?
02 Ukweli Mwingine
04 Huzuni
05 Uchawi
06 Ushirika wa Wasioona Aibu
07 Kuusisimua Mwili
08 Upatanisho wa Mabaya I
09 Upatanisho wa Mabaya II

10 Upatanisho wa Mabaya III
11 Mamlaka - Jumba Kubwa la Mfalme
12 Makusudi ya Kujaribiwa
13 Maono - Ndoto
14 Huduma
15 Mateso
16 Mithali
17 Kitabu cha Yohana

Mafundisho mengine ya ISOB

Mafundisho ya Biblia
Wokovu
Uumbaji - 1
Roho, Nafsi, Mwili
Unajuaje kwamba Biblia ni ya Kweli?
Uumbaji - 2
Roho Mtakatifu wa Milele

Timu Yenye Nguvu kwa watoto

Masomo 13 kutoka katika Kitabu cha Yohana kwa watoto (pamoja na katuni) (Kanda zinatolewa)

Kiambatisho B –Jinsi ya kuendelea katika ISOB
(Masomo yote ya ISOB yanapatikana katika CD ROM)

1. Mahitaji ni yapi?

Tunahitaji Neno na Roho Mtakatifu amdhihirishe Yesu kwetu . Tunahitaji uwepo wa Mungu, siyo tu kanisani, bali pia katika maisha yetu ya kila siku.

Tunamhitaji Mungu na Neno lake litusafishe na kutufanya wanafunzi wa Yesu. Tunahitaji njia ya kivitendo ya kubeba msalaba wetu kila siku na kumfuata Yeye.

Tunahitaji elimu ya Neno ili tushinde mambo magumu tutakayokutana nayo maishani.

Tunahitaji kuwa na uhusiano na wengine katika mwili wa Kristo, kama washauri na wanafunzi.

Tunahitaji kuufikia ulimwengu unaoangamia, na kuuruhusu uwepo wa Mungu utiririke kutoka kwetu hadi kwa watu wengine.

Tunahitaji kuwapa mamilioni ya watu wanaookolewa kila siku pote ulimwenguni, mafundisho yaliyo wazi, rahisi kueleweka. Wanahitaji kujua ukweli ili waweze kukua wasishindwe.

2. ISOB

Ni njia ya kuwafundisha wanafunzi wa Yesu na wahudumu kwa ajili ya Agizo Kuu.

Ni njia ya kuja katika uwepo wa Mungu kwa ajili yako mwenyewe.

Ni njia ya Mungu ya kufanya Neno na Roho Mtakatifu kuwa Mwalimu wako.

Ni njia ya kujifunza jinsi ya kujilisha mwenyewe Neno la Mungu.

Kulipata kwa wingi Neno la Mungu siyo tu suala la kuwa na nidhamu katika kuisoma zaidi Biblia. ISOB itakupatia utaratibu mzuri wa kulifanya Neno la Mungu lihusike kabisa na wewe na pia liwe la kuvutia.

3. ISOB siyo Shule hasa ya Biblia. Inaweza kutumika kama mfumo wa kushauri, watu wanapojifunza pamoja au mtu anapojifunza mwenyewe. Dhana kamili ni kuwawezesha watu wasioweza kwenda Shule ya Biblia kuwa wanafunzi wa Yesu na viongozi. Ni njia rahisi ya kukua katika Bwana. Inaweza kufanyika nyumbani, kanisani, au sehemu yoyote nyingine Bwana atakayotoa. Maelezo haya yatafafanua kwa undani jinsi mfumo huu unavyofanya kazi na hatua unazopaswa kuchukua ili kuanza. Maandiko ambayo kwayo Bwana ameianzisha kazi hii ni haya:

Bwana analitoa neno lake; **Wana wake watangazao habari ni jeshi kubwa** (Zaburi 68:11)

Waefeso 4:11-16 "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; **kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;** hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na

kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo."

Maandiko hayo yananiambia kwamba tunapaswa kuwajenga watakatifu (washauri na wanafunzi) ili waweze kuingia katika huduma.

4. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi kwa mwanafunzi mmoja mmoja:

Kama wewe ni mwanafunzi binafsi, unaweza kutumia masomo haya kama upendavyo. Tunashauri utumie muhtasari wa mtaala.

5. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi mahali ambapo watu wanajifunza kwa pamoja:

Baadhi ya viongozi wa ISOB hupendelea kuwa na vipindi vya kujifunza Biblia katika kikundi tofauti na kuandikisha washauri. Kiongozi anachofanya tu ni kuwa na mahali pa kukutania kila wiki na kisha hufundisha kila somo la ISOB kwa kufuata mpangilio. Nafasi ya kuuliza maswali au kujadiliana inaweza kuwepo. Kiongozi anaweza kuwapa wanafunzi fomu ya maoni waijaze au la.

6. Hivi ndivyo ISOB inavyofanya kazi mahali panapotumika kutolea ushauri:

Tunaona kwamba mfumo wa kushauri siyo tu kwamba unaokoa fedha na muda, lakini unajenga **mahuasiano** ya ajabu kati ya mshauri na mtu mzima. Tunao mpango hapa katika kanisa letu la nyumbani unaoitwa "Light Force" ulio sehemu ya ISOB. Katika mpango huo kuna wastani wa wanafunzi 60 (wenye umri wa miaka 12-14) na washauri (watu wazima) 20. Tuko katika mwaka wa nne na ni baraka kweli.

a. Nia ni kuweza kutoa nakala za kila somo kwa kila mwanafunzi ili kwamba waweze kwenda nazo nyumbani, wazisome huko huko nyumbani na kuleta ripoti wakati kikundi kinapokutana. Kwa kuwa masomo ya ISOB hutolewa kwa gharama nafuu au hata bure, kila mahali ambapo kuna ISOB, wanahimizwa kumruhusu kila mwanafunzi awe na masomo yake mwenyewe. Mwanafunzi anaposoma sura moja, hujaza Fomu ya Maoni ya Mwanafunzi na kumpa mshauri wake. Mshauri siyo lazima awepo wakati mwanafunzi anaposoma sura yake na kujaza fomu yake.

Ni vizuri kubadili badili masomo katika Sehemu ya “Mungu ni nani,” “Kuketi,” “Kuenenda,” na “Kupinga.” Usifanye masomo yote ya “Mungu ni nani” kabla ya kuanza somo la “Kuketi.” Yachanganye.

b. (Ni lazima pawepo na mshauri mmoja kwa kila wanafunzi 3 au 5 - wanafunzi wanaweza kuwa zaidi iwpo mshauri anao muda). Mshauri siyo lazima awe mwalimu au mtu aliyehitimu mafunzo katika Chuo cha Biblia. Mshauri anapaswa tu kuwa mwanafunzi wa Yesu na aliyeazimia hasa kuingia katika huduma ili kuwafikia wengine. Jambo la kukumbuka hapa ni kwamba Roho Mtakatifu na Neno katika kitabu ndio wanaofundisha, mshauri anachofanya tu ni kutia moyo na kutegemeza. Akiweza kujibu maswali, vema. Asipoweza, usiwe na wasi wasi kuhusu hilo. Tafadhali soma masomo yaliyoambatishwa kuhusu uongozi na kushauri.

c. Kisha mshauri humjibu mwanafunzi kwa kujaza fomu ya Maoni ya Mshauri. Majibu yake yanaweza pia kuwepo kwenye fomu ya Maoni ya Mwanafunzi au kwa njia ya maneno machache; au anaweza kuandika maoni yake kwenye karatasi ya kawaida. Ni vizuri mwanafunzi akitunza ripoti yake na maoni ya mshauri mahali pa salama ambapo anaweza kuiangalia wakati ujao.

d. Labda utapenda kuwa na mikutano kila wiki au nusu mwezi pamoja na washauri na wanafunzi katika eneo moja kwa ajili ya ushirika na kujifunza. Tunakutana na kikundi cha "Light Force" kila Jumapili ya kwanza na ya tatu jioni.

e. Wakati mwingine ushauri unaweza kutolewa kwa njia ya barua pepe(e-mail) au kwa njia ya Posta kwa watu walio katika nchi tofauti.

f. Tunapendekeza kwamba orodha ya kupimia ya kila nusu mwezi au kila mwezi itumwe katika ofisi ya nyumbani ili tuweze kuona kazi inavyokwenda na kuiombea huduma na wanafunzi wako.

International School of the Bible (Shule ya Kimataifa ya Biblia)
Marieta, GA. U.S.A.
info@isob-bible.org

ISOB

International School of the Bible
(Shule ya Kimataifa ya Biblia)
Inafundisha Watu Wazae Matunda kwa ajili ya Ufalme wa Mungu



Fomu ya Maoni ya Mwanafunzi

Jina _____ **Tarehe:** _____
Kitabu _____ **Sura ya:** _____

1. Andika hapa mambo yaliyokuvutia zaidi katika sura hii

2. Andika hapa jambo, kama lipo, unalosikia kwamba Mungu anataka ulifanye au ulitii katika sura hii. Kwa maneno mengine, Unajisikia kwamba unataka kufanya nini sasa baada ya kusoma sura hii.

3. Ni jambo gani katika sura hii unalopenda kulifahamu zaidi. Je, una maswali yoyote unayoona kwamba yanahitaji kujibiwa? Andika maswali yako hapa.

4. Andika hapa maombi unayopenda tuombe pamoja nawe kwa mapatano.

Kukua au Kufa
Mfululizo wa Semina

Ni jambo gani lililo muhimu kuhusu agano la damu?

Insert picture

Kitabu cha Kukua au Kufa kitakupeleka katika agano la damu hadi katika uwepo wa Mungu!

Mahitaji yetu yapo katika uwepo wake –
Katika Wafilipi 4:19 tunaambiwa kwamba “Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.”

Mahitaji yetu na kusudi la Yesu la kuufikia ulimwengu huu yanaletwa na utaratibu wa kuzaa matunda unaoanzia katika uwepo wake.

Kukua au Kufa ni kitabu kinachohusu jinsi ya kwenda katika uwepo wa Mungu na kuenenda katika utaratibu wa kuzaa matunda, kufuatana na mpango wa Mungu.